
UFALME WAKO UJE

NOVENA



# MUNGU PAMOJA NASI

*Askofu Mkuu wa Canterbury*

**Sarah Mullally**

UFALME WAKO UJE

NOVENA

Ufalme Wako Uje: Novena
(Kimeandikwa na Askofu Mkuu wa Canterbury Sarah Mullally)
Hakimiliki © 2026 Ufalme Wako Uje (Thy Kingdom Come).
Kimetumika kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa duniani kote.

Nukuu za Maandiko zimetolewa kutoka Biblia Takatifu,
Toleo la New International Version® NIV®
Hakimiliki © 1973, 1978, 1984, 2011 na Biblica, Inc.
Zimetumika kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa duniani kote.

UFALME WAKO UJE

NOVENA

# MUNGU PAMOJA NASI

*Askofu Mkuu wa Canterbury*

**Sarah Mullally**



# Utangulizi

> Matendo 1:14
>
> Wote walidumu kwa moyo mmoja katika maombi, pamoja na wanawake, na Mariamu mama yake Yesu, na ndugu zake.

Tangu mwanzo kabisa wa Kanisa, siku hizi tisa kati ya Kupaa na Pentekoste – yaani Novena – zimekuwa ni wakati wa maombi. Na si maombi ya mtu mmoja mmoja tu, bali maombi ya pamoja, kama wale waumini wa kwanza wa Kanisa.

Na hilo ndilo kusudi la Ufalme Wako Uje, kutuunganisha katika maombi – zaidi ya Wakristo milioni moja katika nchi 172 na madhehebu na mila zaidi ya 85.

Mada ya mwaka huu ni "Mungu Pamoja Nasi", na jinsi Roho Mtakatifu amekuwa akitenda kazi duniani. Na kiini chake, kama kawaida, ni Kuombea Watu Watano, tunapowaombea watu watano ambao ni marafiki, familia, majirani au wafanyakazi wenzetu na bado hawajamfuata Kristo, ili waweze kumjua kama sisi tunavyomjua.

Katika Novena ya kwanza, Mitume hawakuomba Mungu aipeleke Injili duniani. Waliomba kuja kwa Roho Mtakatifu, ili awabadilishe na kuwapa nguvu ya kwenda kushiriki Habari Njema.

Na hivyo ndivyo Novena ya mwaka huu itakavyokuwa pia.

Kwa sababu maombi si tu kumwomba Mungu abadilishe ulimwengu. Nimegundua kwamba pia ni kumwomba Mungu atubadilishe na sisi.

Maombi humbadilisha anayesali.
Mungu hutubadilisha, kama mfinyanzi anavyotengeneza udongo, akitutengeneza upya kuwa katika sura iliyo sahihi zaidi, sura ya mfano wake. *"Kama udongo mkononi mwa mfinyanzi, ndivyo mlivyo mkononi mwangu."* (Yeremia 18:6).

Na kama tutakavyoona katika masomo yajayo, Mungu anataka kutugeuza kuwa watu wanaofanya mabadiliko tunayotaka kuyaona duniani.

Kwa sababu kama kweli tunamaanisha tunachoombea, basi maombi yetu lazima yaambatane na matendo, kama Mitume walivyotenda mara tu baada ya Pentekoste, wakitiwa nguvu na Roho Mtakatifu. Ikiwa tunatamani kwa dhati watu wetu watano wakutane na Mungu, kwa nini isiwe kupitia sisi?

Kwa msaada wa Mungu, tunaweza kuwa jibu la maombi yetu wenyewe.

Kama alivyoandika Teresa wa Avila:

*'Kristo hana mwili mwingine ila wako,*
*hana mikono wala miguu duniani*
*ila miguu na mikono yako,*
*macho yake ni yako anayotumia*
*kutazama dunia hii kwa huruma,*
*miguu yake ni yako anayotumia*
*kutembea na kufanya mema,*
*mikono yake ni yako anayotumia*
*kuibariki dunia.*
*Kristo hana mwili duniani ila wako.'*

Tunaweza kuwa mikono ya Kristo kwa wale wanaohitaji.

Kwa hiyo, katika Novena hii, tutaomba tuwe chombo cha kuwakutanisha watu wetu watano na upendo wa Mungu, ili wamjue kupitia sisi.

Lakini pia tutagundua kwamba sisi wenyewe tutabadilishwa na Roho Mtakatifu, na kuumbwa upya kuwa na sura inayofanana zaidi ya Mungu.

***Askofu Mkuu wa Canterbury,***
***Sarah Mullally***

## Ombea Watu Watano

1.
2.
3.
4.
5.



# Siku ya Kunyakuliwa

## *Roho wa Ahadi*

Matendo 1:6-11

6 Walipokusanyika wakamwuliza, *'Bwana, je, wakati huu*
*utaurudisha ufalme kwa Israeli?'*
7 Akawaambia, *'Si juu yenu kujua nyakati wala majira*
*ambayo Baba ameweka kwa mamlaka yake mwenyewe.*
8 *Lakini mtapokea nguvu, atakapowajilia Roho Mtakatifu;*
*nanyi mtakuwa mashahidi wangu Yerusalemu, na katika*
*Uyahudi wote na Samaria, na hata miisho ya dunia.'*
9 Baada ya kusema hayo, akachukuliwa juu mbele ya
macho yao, na wingu likamficha wasimwone.



Nadhani wakati mwingine sote huwa tunajihisi kuwa Hatuna nguvu. Tunajihisi hatuna uwezo wa kubadilisha dunia, au hata kubadilisha maisha yetu wenyewe. Hivyo tunamuuliza Mungu, 'Utafanya nini? Je, hatimaye utaurudisha Ufalme wako?'

Na kisha tunapokea jibu la kukatisha tamaa, 'Si juu yenu kujua.'

Lakini hata kama tunajihisi kuwa wanyonge kiasi gani – hata kama tunajihisi tuko gizani na mambo mengi hatufahamu yatakuwaje – tunaweza kupata faraja katika maneno ya Kristo ya mwisho duniani. Roho atakapokuja juu yenu, 'mtapokea nguvu'. Na si nguvu tu yeyote, bali nguvu ya kueneza habari njema katika kila sehemu ya dunia.

Unaweza kuwa unajiuliza, 'Mbona bado najihisi mnyonge, ninawezaje kujua kwamba ahadi hii ni ya kweli?'

Naam, wala hatuhitaji kutazama mbali bali unahitaji kujitazama tu wewe mwenyewe. Wewe, na wasomaji wote wa Novena hii, ambao mnatoka kila kona ya dunia, katika nchi zaidi ya 172. Ndani yenu, katika Ushirika wa Anglikana, katika kanisa lolote ulimwenguni, tunaweza kuona kwamba ahadi yake ilikuwa kweli, na kwamba habari njema imefika hadi mwisho wa nchi. Waliotutangulia ni hakika walipewa nguvu za Roho Mtakatifu kuwa mashahidi wa Kristo kwa ulimwengu. Na – kwa hiyo – nasi tumekuwa mashahidi pia.

Na ikiwa tumepewa nguvu za kufika mwisho wa nchi, hakika tumepewa nguvu za kutuwezesha kuwafikia watu wetu watano.

**Basi hebu tuombee ili tuweze kuzitambua nguvu za Roho Mtakatifu zilizo ndani yetu, na haijalishi Mungu anaweza kuacha mambo mengi kiasi gani tusiyajue, tuzitumie nguvu hizo kushiriki habari njema na watu wetu Watano.**



# *Roho Anakaa juu ya Uumbaji*

> Mwanzo 1:1-5
>
> [1] Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi. [2]Nchi
> ilikuwa ukiwa na utupu, giza lilikuwa juu ya vilindi, na
> Roho wa Mungu alikuwa akitanda juu ya maji.
>
> [3]Mungu akasema, *'Na kuwe na nuru,'* nayo nuru ikawa.
> [4]Mungu akaiona nuru kuwa njema, akaitenga nuru na
> giza. [5]Mungu akaiita nuru 'mchana,' na giza akaliita 'usiku'.
> Ikawa jioni, ikawa asubuhi – siku ya kwanza.

Hebu fikiria, fikiria kichwani kwako, giza kali kabisa kuwahi kutokea.

Giza ambalo si tu kwamba halijaguswa na mwanga, bali giza ambalo hata huo mwanga haujawahi kuwepo.

Lakini hata katika giza hilo – giza kali lililowahi kuwepo, au litakalowahi kuwepo, wakati ambapo vitu haviwezi kuwa vyeusi zaidi ya hapo – bado kulikuwa na tumaini. Roho alikuwepo, akitanda juu ya maji.

Wakati wowote ninapojikuta gizani, jambo hili linanipa faraja, kwamba Mungu alikuwepo mwanzo, na Roho wake yuko nasi leo, haijalishi hali yetu ipoje.

Lakini wakati mwingine inaweza kuwa vigumu kuhisi uwepo huu. Nyakati kama hizo, utaweza kuhisi uwepo wa Roho vizuri zaidi kupitia wengine.

Nilipokuwa nafanya kazi kama muuguzi, nilikuwa katika kitengo cha huduma kwa wagonjwa mahututi, niliwaona watu wakipitia nyakati za giza kuu, wakikutana na mshtuko na huzuni ya maisha yao kukatishwa. Nilichogundua ni kwamba watu hao hawakuwa wakiomba kupata majibu ambayo hakuna mtu angeweza kuyatoa – waliomba tu mtu awepo karibu, mtu awe pamoja nao. Si tu kuwa pamoja naye kimwili, bali kwa kiroho pia.

Mungu hutenda kazi kupitia sisi – watu wanaweza kumhisi Roho wake kupitia sisi – naye anatutaka tuwe pamoja na wale wote ambao wapo gizani.

Kama Isaya alivyotamka, *'Roho wa Bwana amenituma kuwafunga wagonjwa wa moyo, kuwafariji wanaoomboleza, na kuwaachilia wafungwa gizani.'* (Isaya 61:1-2)

**Kwa hiyo tuombe yafuatayo, tuombe iwapo mtu yeyote kati ya watu wetu Watano atajikuta yuko gizani, tuweze kuwa karibu pamoja naye katika wakati huo, huku tukishiriki uwepo wa Roho Mtakatifu pamoja naye.**



# *Roho wa Neema*

Ruthu 1:16-18

16 Lakini Ruthu akajibu, *'Usinisihi nikuache au nirudi*
*nyuma yako. Uendako nienda, ukakako nikae. Watu wako*
*watakuwa watu wangu, na Mungu wako atakuwa Mungu*
*wangu.* 17 *Ufako nifae, na hapo nitazikwa. Bwana anifanyie*
*vibaya zaidi ya hayo, kama hata kifo kikitutenga mimi nawe.'*

18 Naomi alipogundua kuwa Ruthu alikuwa amedhamiria
kwenda naye, akaacha kumsihi.

Nadhani haikuwa rahisi kwa Ruthu kusema maneno haya. Kwani ilimaanisha kuondoka nyumbani kwao Moabu, na kuacha familia yake yote na kila kitu alichokijua maishani mwake hadi kufikia wakati huo.

Bila kusahau kwamba siku zote sio rahisi kujitoa kikamilifu kwa ajili ya mtu mwingine, hata pale tunapokuwa kwenye nyakati zetu nzuri – na ni vigumu zaidi kufanya hivyo tunapokuwa tunakataliwa. Na hivyo ndivyo Ruthu alivyokuwa akitendewa.

Naomi alikuwa anateseka sana kutokana na msiba. Alikuwa amempoteza mume wake na wanawe wote wawili. Alikuwa tayari amezeeka sana kuweza kuolewa tena, achilia mbali kuzaa watoto wengine. Naye aliamini kwamba Mungu alikuwa amegeuka dhidi yake. Hata akabadilisha jina lake kutoka Naomi (maana yake mrembo) hadi kuwa Mara (maana yake mtu mwenye uchungu): *'Niite Mara, kwa sababu Mwenyezi Mungu amenifanya maisha yangu kuwa machungu sana.* […] *Kwa nini uniite Naomi? Bwana amenitesa; Mwenyezi Mungu amenitea misiba.'* (Ruthu 1:20-21)

Aliwasukuma mbali wale waliokuwa karibu yake, sote tunajikuta tukifanya hivyo tunapokuwa kwenye shimo refu la kukata tamaa – lakini Ruthu aliona hayo yote, na hakutaka kumtelekeza. Ruthu alijaa Roho wa neema.

Katika upendo wake kwa Naomi, tunaweza kuona sehemu kidogo ya upendo wa Mungu kwetu sisi usio na masharti. Kupitia Yesu Kristo, Mungu alionyesha kujitoa kwake kwa wanadamu, naye alituambia, *'Popote muendako, nami nitaenda; utakapokufa, nami nitakufa.'* Naye yuko nasi hata hivi leo kila mahali tuendako, tangu mwanzo hadi mwisho wa maisha yetu, kupitia Roho wake Mtakatifu.

Hata hivyo, kadri siku zinavyosonga, ndivyo tunavyozidi kugeuka mbali naye, kupitia yale tunayofikiria na yale tunayoyasema, tunayofanya na kushindwa kufanya – tukizidi kugeuka mbali na Ruthu – lakini kila siku anajitoa kwetu kupitia Roho Mtakatifu. Na hiyo ndiyo neema: upendeleo usiostahili kutolewa, na usio na masharti.

Neema ndiyo kitu alichohitaji Naomi. Ndiyo wanayohitaji wanadamu. Na ndiyo wanayohitaji watu wetu Watano pia.

**Na hivyo tuombe kwamba Roho wa neema atuonyeshe – hata wakati mgumu (hasa wakati mgumu) – jinsi ya kuwa wenye neema kwa watu wetu Watano, jinsi ya kujitoa kwa ajili ya ustawi wao, na kushuhudia upendo wa Mungu kwetu sote usio na masharti.**



# *Roho wa Kusikiliza*

> 1 Samweli 3:1-11
>
> […] [3]Samweli alikuwa amelala ndani ya nyumba ya Bwana, pale ambapo sanduku la Mungu lilikuwa. [4]Ndipo Bwana akamwita Samweli. […]
>
> [8]Bwana akamwita mara ya tatu, *'Samweli!'* Samweli akainuka akamwendea Eli akasema, *'Niko hapa; umeniita.'*
>
> Ndipo Eli akagundua kwamba Bwana ndiye aliyekuwa akimwita yule kijana. [9]Kwa hiyo Eli akamwambia Samweli, *'Nenda, ukalale, na akikuita, jibu, "Sema, Bwana, kwa kuwa mtumishi wako anasikiliza."'* Basi Samweli akaenda akalala mahali pake.
>
> [10]Bwana akaja akasimama pale, akamwita kama mara nyingine, *'Samweli! Samweli!'*
>
> Ndipo Samweli akasema, *'Sema, kwa kuwa mtumishi wako anasikiliza.'* […]

Unajikuta unaomba vizuri ukiwa wapi? Je, ni ukiwa kanisani, au unapotembea katika mazingira yenye miti na ya asili, au labda ukiwa nyumbani, kitandani, mahali penye ukimya?



Sote tuna njia zetu za kujiweka kwa namna tunayoona inatufaa zaidi, namna inayoturuhusu kusikia neno la Mungu.

Kwangu mimi, kuna mahali nyumbani kwangu ambapo huwa ninakwenda kila asubuhi kuomba, kusoma Biblia, kusoma Maombi ya Asubuhi, au kukaa kimya tu. Lakini zaidi ya hayo, kufanya hivyo inakuletea ratiba nzuri kwa ujumla – unakuwa na ratiba inayompa Mungu nafasi na wakati wa kusema, na nafsi yako na pia kuwa na nafasi ya kusikiliza.

Kwa Samweli, inaonekana alihitaji kulala chini, labda ilibidi iwe ni usiku, na – sio jambo la kushangaza – ilikuwa ni ndani ya Patakatifu pa Patakatifu, mahali palipokuwa na Sanduku la Agano, kwa ujumla ilikuwa ni vizuri kwake.

Lakini Samweli aliposikia sauti ya Roho, hakuelewa kilichokuwa kinaendelea, au kwa nini alikuwa akijibu kwa njia isiyofaa – ilikuwa kana kwamba alikuwa akitumia redio ya mawasiliano iliyopokea na kutuma mawimbi kwa masafa tofauti – na huenda alijisikia kama alikuwa akifanyiwa utani.

Lakini alipata ushauri muhimu.

Eli hakuonyeswa vyema katika kitabu hiki cha Biblia, lakini katika hadithi hii ana jukumu muhimu sana. Alimfundisha Samweli jinsi ya kumsikiliza Roho: kurudi na kulala chini, mahali pake pa kwanza – alimfundisha kurekebisha redio yake ili ikamate mawimbi sahihi – na pia iweze kujibu kwa njia sahihi. Matokeo yake ni kwamba, alimsaidia kutambua jinsi ya kuomba.

Najiuliza, je kama watu wetu Watano wangesikia sauti kama Samweli alivyosikia, je, wangejua ni nani au ilikuwa nini, au jinsi ya kujibu?

Kwa sababu Mungu anaweza kuwa anawaita leo – tena, nina hakika anawaita hivi sasa – na ni juu yetu sisi kufanya jukumu la Eli.

**Na hivyo tuombe kwamba tuweze kuwasaidia watu wetu Watano kusikia wito huo unaowaita, na tuwahimize kuisikiliza – kwa sababu, kama Samweli, kusikiliza wito huo kutabadilisha maisha yao.**



# *Roho wa Ujasiri*

> Waamuzi 6:11-14
>
> [...] 12Malaika wa Bwana alipomtokea Gidoni, akasema, *'Bwana yu pamoja nawe, shujaa hodari.'*
>
> 13Gidoni akamjibu, *'Samahani, bwana wangu, lakini ikiwa Bwana yu pamoja nasi, kwa nini haya yote yametupata? Wako wapi maajabu yake yote ambayo baba zetu walituambia waliposema, "Je, si Bwana aliyetutoa Misri?" Lakini sasa Bwana ametutelekeza na kututia mikononi mwa Midiani.'*
>
> 14Bwana akamgeukia akasema, *'Nenda kwa nguvu uliyonazo, na uwakomboe Waisraeli kutoka mikononi mwa Midiani. Je, si mimi ninayekutuma?'*

'K*ama Bwana yu pamoja nasi, kwa nini haya yote yametupata?'*

Nihisi kutakuwa na watu wanaosoma sehemu hii ambao wanauliza swali kama hili ambalo aliuliza Gidoni.

Inaeleweka kabisa kwa nini Gidoni alijisikia kutelekezwa na Mungu, kwa nini alihisi uchungu sana dhidi yake, na kwa nini aliuliza yako wapi maajabu ya Mungu na kwa nini hawezi kuyafanya lolote leo.



Na inaeleweka kwa nini sisi huenda wakati mwingine tujisikie hivyo leo.

Katika nyakati ambapo tunajisikia kutokuwa na tumaini na kwamba hakuna chochote tunachoweza kufanya ili kusaidia, tutakuwa tunataka Mungu atatue jambo hilo. Lakini Mungu anatuambia nini badala yake (hata wakati na labda hasa wakati tunapomchukia)?

'Songa kwa nguvu uliyonazo ... Je, si mimi ninayekutuma?'

Anatutuma tufanye lile ambalo tungetaka yeye afanye.

Kama muuguzi katika wodi ya wagonjwa wa saratani, nilifanya kazi mahali ambapo watu mara nyingi hujisikia wanyonge sana. Mahali hapo dunia haikuwa na suluhisho, na watu mara nyingi waliuliza, 'Kwa nini?': kwa nini Mungu wa upendo wake anaruhusu mateso kama haya, na, ikiwa Yesu alimponya mwenye ukoma, kwa nini hawezi kuniponya mimi?

Lakini ingawa mambo yanaweza kuonekana magumu na yasiyo na tumaini, pia ni mahali ambapo kitu cha ajabu kinaweza kutokea.

Ni mahali ambapo, hata kama hakuna tiba ya kimwili, hata kama hatuna majibu yote, tunaweza kutembea pamoja na watu wanajaribu kushinda kukata kwao tamaa, na kuwasaidia kuishi maisha kwa ukamilifu wake. Tunaweza kuwa pamoja nao katika mateso yao, kama Mungu alivyo.

Hivi leo, tunaweza kujisikia kutokuwa na tumaini kwa watu wetu Watano, tukihisi hakuna chochote tunachoweza kufanya kuwavuta kwa Mungu – lakini Roho anatuagiza tusikate tamaa. Anatuambia tusisubiri mpaka Mungu atende, bali anatutuma kwa nguvu tuliyonayo, akituambia tufanye tuwezalo – kwa sababu, iwe tunatambua au la, 'Bwana yu pamoja nawe.'

**Basi tuombe tusishindwe kuchukua hatua, bali tuitikie kwa ujasiri wito wa Roho anayetutuma kwa watu wetu Watano. Kwa maana Mungu atatenda kazi kupitia sisi, kwa nguvu tuliyonayo.**



# *Roho na Sauti Ndogo na Tulivu*

> 1 Wafalme 19:9b-13
>
> [9]Neno la Bwana likamjia: *'Unafanya nini hapa, Eliya?'*
>
> [10]Akajibu, *'Nimekuwa mwenye bidii sana kwa Bwana Mungu Mwenye Nguvu Zote. Waisraeli wamekataa agano lako, wamezibomoa madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga. Nimebakia peke yangu, na sasa wananitafuta kuniua mimi pia.'*
>
> [11]Bwana akasema, *'Nenda nje, usimame mlimani mbele ya Bwana, kwa maana Bwana atapita.'*
>
> Ndipo upepo mkubwa wenye nguvu ukapasua milima na kuvunja miamba mbele ya Bwana, lakini Bwana hakuwa ndani ya upepo. Baada ya upepo kukawa na tetemeko la ardhi, lakini Bwana hakuwa ndani ya tetemeko. [12]Baada ya tetemeko ukaja moto, lakini Bwana hakuwa ndani ya moto. Baada ya moto ikaja sauti ndogo ya utulivu. [13]Eliya alipoisikia, akajifunika uso wake na joho lake, akatoka nje akasimama kwenye mlango wa pango.
>
> Ndipo sauti ikamwambia, *'Unafanya nini hapa, Eliya?'*



Sijui wewe; lakini kwangu mimi, jibu la Eliya linaonekana kuwa ni jibu la mantiki kabisa!

Mungu alikuwa amemuuliza kwa nini yuko pale, naye akatoa jibu la kweli, na la busara sana. Nisingeshangaa kama mtu asingeenda kujificha akipitia katika hali kama hiyo.

Lakini ni wazi Mungu alitaka Eliya afikirie upya.

Kwa hiyo Eliya akaambiwa atoke nje – akaona milima ukipasuka, ardhi ikitetemeka chini yake, na moto mkali – yote hayo, kisha Roho anarudi na kunong'ona kwa sauti ndogo swali lile lile.

Hii si kama hadithi ya Samweli na Eli. Eliya hana tatizo la kuwasiliana na Mungu – anaweza kumsikia kwa uwazi, kumuelewa, kumuitikia – na Mungu anatumia hilo kumbadili.

Kwa sababu Mungu alikuwa haombi kupewa taarifa – tayari alilikuwa anajua kwa nini Eliya alikuwa pale. Hili lilikuwa swali ambalo tayari alikuwa na jibu lake, alikuwa akijaribu kumwambia Eliya aache visingizio, atoke mafichoni, na achukue hatua..

Hatimaye Eliya alielewa ujumbe huo.

Binafsi najiuliza kitu kimoja – ni swali gani ambalo kila mmoja wetu analazimika kulijibu mara kwa mara?

Kwangu mimi, siku zote swali hilo limekuwa ni kama ninajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kuzitumia karama alizonipa Mungu.

Labda ni hivyo kwako pia, au labda kuna swali linalokusumbua kuhusu mmoja kati ya watu wako Watano – kwa nini sijawahi kumuuliza kuhusu masuala ya imani? Kwa nini sijamualika kanisani? – kwa sababu kama swali hilo linarudi mara kwa mara kwako, basi tunajua Mungu atakuwa na sababu!

**Basi tuombe kwamba, swali lolote ambalo Roho anatunong'oneza kwa sauti ya utulivu – hasa kama linamhusu mtu mmoja kati ya wale watu wetu watano – basi tuweze kulijibu kama Mungu anavyotaka: na si kwa kulipuuza, si kwa kuacha kulisikiliza, si kwa visingizio – bali kwa kuchukua hatua.**



# *Roho na Uongozi*

Waamuzi 4:3b-5

3 Wakalia wakimwomba Bwana msaada.

4 Wakati huo Debora, nabii, na mke wa Lapidothi,
alikuwa akiiongoza Israeli. 5 Alikuwa akikaa chini ya
mtende wa Debora kati ya Rama na Betheli katika nchi
ya milima ya Efraimu, na Waisraeli walimwendea ili atoe
hukumu ya mashauri yao.

Huenda umegundua kwamba, tunakuwa tunaomba, majibu huwa hayaji kila mara kwa namna tunavyotarajia. Siyo lazima tusikie sauti ya Mungu kama Samweli au Eliya walivyosikia – badala yake, tunamwona Roho akitenda kazi kupitia mtu mwingine, akizungumza kupitia wao, na hapo ndipo tunapata mwongozo.



Katika simulizi hii, Waisraeli walikuwa wakimlilia Mungu wakiomba msaada, na walitambua kwamba Roho alikuwa akizungumza nao kupitia Debora, hivyo wakamgeukia kwa uongozi.

Debora hakulazimisha kuwa kiongozi wa Israeli. Alijiweka tu tayari, akajitolea kwa yeyote aliyemhitaji, na akawahudumia. Kama vile Baba ambavyo anakuwa yuko tayari kwa lolote kwa ajili yetu kila tunapotaka kumuomba. Na kama vile Mwana alivyokuja, si kutumikiwa, bali kutumikia.

Kama watumishi wote wa Mungu, huwa ninajaribu kuiga uongozi huu wa kiroho – huwa sijaribu kulazimisha watu kufuata njia yangu, bali najaribu kuwainua wengine, kuwajengea ujasiri, na kuwasaidia kutumia vipawa vyao walivyopewa na Mungu.

Katika makanisa ya mtaani kwetu, tuna viongozi walioko karibu nasi – makuhani na wachungaji, waliojazwa na Roho Mtakatifu, ambao wako tayari kutuhudumia, kutuongoza, na kuibua mema yaliyo ndani yetu.

Hivyo basi, tuwatafute, kama Debora alivyotafutwa na Wana wa Israeli hapo zamani, kwa sababu tunapojaribu kuelewa jinsi ya kuwaongoza wale watu wetu Watano kwenye imani, tunaweza kugundua kwamba Roho anazungumza nasi kupitia wao.

**Tuwaombee viongozi wa makanisa, wachungaji na waliowekwa wakfu, ili kwa kusikiliza sauti ya Roho, waweze kutusaidia kusambaza upendo wa Mungu kwa wale watu wetu Watano.**



# *Roho wa Ukuu*

> Mathayo 3:13-17
>
> [13] Kisha Yesu akatoka Galilaya akaenda mpaka Yordani kubatizwa na Yohana Mbatizaji. [14] Lakini Yohana akajaribu kumzuia, akisema, *'Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, halafu wewe wanijia mimi?'*
>
> [15] Yesu akamjibu, *'Acha iwe hivyo sasa; kwa maana ndivyo ipasavyo ili kutimiza haki yote.'* Ndipo Yohana akakubali.
>
> [16] Mara tu baada ya Yesu kubatizwa, aliinuka kutoka majini. Wakati huo huo mbingu zikafunguka, naye akaona Roho wa Mungu akishuka kama njiwa na kutua juu yake. [17] Na sauti kutoka mbinguni ikasema, *'Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa naye.'*

Kama kuna neno moja linaloelezea simulizi hii vizuri, basi ni hili – unyenyekevu.

Kipindi cha Krismasi, Muumba wetu alijinyenyekeza, si tu kwa kuwa sehemu ya uumbaji Wake, bali kwa kuingia ulimwenguni katika hali ya chini kabisa, akazaliwa kwenye zizi la wanyama na kulazwa kwenye hori.

Katika Ijumaa Kuu, hakujinyenyekeza tu kwa kukubali hata kufa kama viumbe Wake, bali pia aliruhusu kudhalilishwa hadharani na kupitia mateso ya msalaba.

Na hapa kwenye ubatizo Wake, alikubali kubatizwa, kutakaswa kiroho na mtu ambaye alimuumba—kana kwamba alikuwa na dhambi kama viumbe Wake.

Ingekuwa vigumu kuamini kama isingekuwa kweli imetokea.

Na hii si ishara tu — unyenyekevu ni kiini cha ukuu wake juu ya uumbaji wote. Kwa maana ni baada tu ya kujinyenyekeza kwake wakati wa ubatizo ndipo Roho wa ukuu aliposhuka juu ya Yesu, na kumtangaza kuwa Mwana wa Mungu.

Kristo anatuonyesha kwamba, ndani ya Mungu, ukuu na unyenyekevu ni kitu kimoja, ingawa vinaonekana kupingana.

Kama Wakristo, tunapaswa kushuhudia unyenyekevu huu, kwa sababu kama alivyofanya Kristo, tumeitwa kuwahudumia wengine.

Nikiwa kama muuguzi, kama kuhani, na kama Mkristo wa kawaida tu, nimeitwa kuosha miguu ya watu wengine. Yesu aliwaosha miguu wanafunzi Wake, na anatutaka tufanye vivyo hivyo kwa wengine — ikiwemo wale watu wetu Watano. Iwe ni kuosha miguu yao kabisa kwa maji au kuiosha kama lugha ya mfano tu, kiini cha kauli hiyo ni kuwahudumia na kuwajali wengine — lakini zaidi ya yote, ni unyenyekevu.

Ni unyenyekevu wetu ndiyo utakaomfanya Roho ashuke juu yetu, kwa maana 'Ajiinuaye atashushwa, na ajinyenyekezaye atainuliwa.' (Mathayo 23:12)

**Basi na tuombe Roho wa ukuu atupe unyenyekevu wa kweli, ili tuwahudumie wale watu wetu Watano kwa moyo wa utumishi, kama Kristo alivyotuhudumia sisi.**



# *Roho wa Uinjilisti*

> Matendo 8:26-35
>
> [...] 29 Roho akamwambia Filipo, *'Nenda karibu na gari lile, ukae karibu nalo.'*
>
> 30 Kisha Filipo akakimbilia lile gari na akamsikia mtu akisoma chuo cha nabii Isaya. Akamuuliza, *'Je, unaelewa unachosoma?'*
>
> 31 Yule mtu akasema, *'Nitawezaje kuelewa kama hakuna mtu atakayenifafanulia?'* Basi akamwalika Filipo apande aketi pamoja naye [...]

Kila siku tunakutana na watu wapya. Hatumsalimii kila mtu na kuanzisha mazungumzo naye — kama tungefanya hivyo, tusingeweza kupata muda wa kufanya lolote! Lakini huwa najiuliza kama hiyo ndiyo sababu halisi ya kunyamaza kwetu.



Nadhani ni vigumu kwa watu kutoka mbele ya mtu asiyemfahamu. Na ni vigumu zaidi pale ambapo mtu huyo anakuwa tofauti na sisi. Ikiwa hakuna jambo linalotuunganisha, hata kusema 'hujambo' inaweza kuwa changamoto, achilia mbali kumfuata kuwafuata na kumuuliza anasoma nini au kitu kama hicho.

Lakini hivyo ndivyo Filipo alivyofanya. Huenda alifikiri, 'Mimi mtu wa kawaida kutoka kijiji cha wavuvi Galilaya, ninawezaje kuhusiana na afisa wa kifalme kutoka Ethiopia?'

Lakini Roho alikuwa na jibu: nenda tu, na uone kitakachotokea. Hatimaye Filipo aliweza kumfundisha mtu huyu maana ya ndani kabisa ya unabii wa Isaya.

Huwa tunazungumza sana leo kuhusu kuwa mabalozi bora wa Kristo. Lakini hapa Roho anatukumbusha jambo jepesi ambalo liko wazi kabisa: hatuwezi kumzungumzia Mungu kama hatuko kwenye mazungumzo naye.

Roho hakumpa Filipo mbinu za kuzungumza (hakika Filipo angefurahia kupata mbinu hizo) — alimpa agizo moja tu: 'Nenda kwenye gari hilo na ukae karibu nalo.' Mungu alimwamini Filipo kuendelea kutoka hapo.

Vivyo hivyo, Roho anatuita nasi leo. Sio kuzungumza na kila mtu, bali angalau kuzungumza na wale watu wetu Watano. Mungu hatuambii nini cha kusema nao au namna ya kusema nao — anataka tu tuanze mazungumzo nao. Na kwa sababu ni rafiki zetu na wanafamilia wenzetu, itakuwa ni rahisi kwetu kuliko ilivyokuwa kwa Filipo – hata kama hatutakuwa na bahati ya kutosha ya kukutana na kusoma Isaya!

**Basi na tuombe ujasiri wa kusikiliza na kuitikia wito wa Roho — kujitokeza na kuanza mazungumzo na yeyote kati ya watu wetu Watano, hata kama tunajihisi kuwa hatujajiandaa. Kwa sababu Mungu anatuamini kusonga kutokea hapa.**



# *Roho wa Vizazi Vyote*

2 Timotheo 1:3-7

[3] Namshukuru Mungu, ninayemtumikia kama mababu zangu walivyofanya, kwa dhamiri safi, ninapokukumbuka katika maombi yangu usiku na mchana.

Namshukuru Mungu ninayemtumikia, kama mababu zangu walivyofanya, kwa dhamiri safi, kwa kuwa usiku na mchana
nakukumbuka daima katika maombi yangu. [4]Nikikumbuka
machozi yako, ninatamani sana kukuona, ili nijazwe furaha.
[5]Nakumbushwa imani yako ya kweli, ambayo kwanza iliishi ndani ya bibi yako Loisi na mama yako Eunike, na nina hakika kwamba sasa anaishi ndani yako pia.

[6] Kwa sababu hii nakukumbusha uichochee iwake tena karama
ya Mungu iliyo ndani yako kwa kukuwekea mikono. [7]Kwa maana
Roho ambaye Mungu ametupa hatufanyi kuwa waoga, bali hutupa nguvu, upendo, na kiasi.

Miaka kadhaa iliyopita nilikuwa hospitalini kwa ajili ya upasuaji. Ingawa nilikuwa nimetumia miongo mingi kama muuguzi, sikuwahi kuwa mgonjwa, wala sikuwahi kupewa dawa ya usingizi wa jumla.

Badala ya kujisikia mwenye utulivu na mwenye kujiamini, nilikuwa ni mwenye



wasiwasi na hofu. Nilipokuwa nimelala pale nikisubiri kulazwa usingizi, nilichotamani zaidi ni mtu ashike mkono wangu.

Hilo lisingepunguza hatari iliyopo mbele, wala lisingenifanya nipone, lakini lingenihakikishia kwamba sikuwa peke yangu.

Sote tunajua maana ya kuwa mpweke. Kuhisi kutengwa (hata tunapozungukwa na watu wengine) na kutamani uhusiano wa karibu wa kibinafsi.

Kwangu inaonekana kama mtume Paulo alikuwa anajihisi vivyo hivyo. Alikuwa akiandika barua hii akiwa gerezani — inadaiwa kuwa ndiyo ya mwisho kabla ya kuuawa kwake — na hamu yake ya kumwona Timotheo inaonekana wazi. Naweza kumfikiria akitamani kukumbatiwa, au angalau kushika mkono wa mtu.

Hatuwezi kudharau umuhimu wa kugusa. Kwa sababu kugusa ni mojawapo ya njia ambazo Roho Mtakatifu hufanya kazi duniani.

Kama Paulo asemavyo, Roho — yaani zawadi ya Mungu — ilimjia Timotheo kupitia Paulo, alipoweka mikono yake juu yake. Na ilikuja kwetu sote pia kupitia mguso katika ubatizo wetu.

Kupitia ajabu ya kugusa, Roho Mtakatifu amesambazwa kati yetu na kupitishwa kutoka kizazi hadi kizazi, katika nyakati zote, tangu wakati wa Paulo hadi sasa, na kuendelea hadi siku zijazo.

Roho wa vizazi vyote — asiye na umbo, asiye na mipaka ya wakati — huja kwetu katika nafasi ndogo ya nafasi na wakati, tunapogusana sisi kwa sisi.

Na tunapaswa kushiriki zawadi yake, ikiwa tunaweza, na wale watu wetu Watano — wale ambao, kama Paulo, tumekuwa tukiwakumbuka daima katika maombi yetu.

**Basi na tuombe kwamba, wakati wowote wale watu wetu Watano wanapohisi upweke, tuwepo kwa ajili yao kwa kuwashika mkono, kuweka mkono begani, au kuwapa kumbatio, kulingana na kinachofaa na kinachokubalika, tukiwashirikisha faraja ya Roho Mtakatifu.**



# Pentekoste

## *Roho wa Ahadi*

> Matendo 2:1-4
>
> 1 Siku ya Pentekoste ilipowadia, walikuwa wote mahali pamoja.
> 2 Ghafla sauti kama ya upepo mkali ikatoka mbinguni na kuijaza
> nyumba yote waliyokuwa wameketi. 3 Wakaona kitu kama ndimi
> za moto zikigawanyika na kutua juu ya kila mmoja wao. 4 Wote
> wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema lugha nyingine
> kama Roho alivyowawezesha.

Wimbo huu wa zamani, *"Njoo, Roho Mtakatifu, sukuma nafsi zetu na uzitie mwanga kwa moto wa mbinguni…"*, uliimbwa katika kutawazwa kwa Charles III, muda mfupi kabla hajapakwa mafuta na Roho Mtakatifu. Mwanzo uliandikwa kwa lugha ya Kilatini, lakini uliimbwa katika lugha za asili za Uingereza (Kiingereza, Kiwelsh, Kigaeli cha Scotland na Kiayalandi), ukikumbusha lugha nyingi zilizozungumzwa na mitume katika Pentekoste ya kwanza — na uliita Pentekoste mpya kwa siku ya leo.



Kwa hakika, wimbo huu umeimbwa katika kila tukio la kutawazwa kwa wafalme wa Uingereza tangu mwaka 1625, kwa sababu imekubalika kwamba mfalme hawezi kubeba uzito wa wito wake peke yake — anahitaji nguvu inayotoka kwa Roho mwenye nguvu.


Na sisi sote tunahitaji msaada huo pia kwa kazi zilizo mbele yetu — hasa katika kushirikisha upendo wa Mungu na wale watu wetu Watano.

Hilo ndilo tumekuwa tukiliombea kwa siku hizi kumi na moja zilizopita — kwamba wale watu wetu Watano wakutane na Mungu, na wafanye hivyo kupitia sisi. Kupitia ujasiri wetu wa kuanzisha mazungumzo nao, hata pale tulipohisi hatuko tayari. Kupitia unyenyekevu wetu, tuwahudumie kwa moyo wa utumishi. Kupitia faraja yetu wanapojikuta wako gizani au peke yao. Kupitia neema yetu, tukijitoe kwa ustawi wao hata pale inapokuwa vigumu kwetu kufanya hivyo. Kupitia mwongozo wetu, tuwasaidie kusikia na kuitikia wito wa Mungu. Na zaidi ya yote kupitia matendo yetu, tujibu sauti tulivu ya Roho na kuwashirikisha watu wetu Watano upendo wa Mungu sisi wenyewe.

Tukifanya yote tuliyoomba, wale watu wetu Watano hawatakutana tu na Mungu kupitia sisi.

Bali sisi wenyewe pia tutakutana na Mungu kwa undani zaidi, na kubadilishwa na Roho Wake kuwa watu wenye neema, unyenyekevu, faraja, kusikiliza, ujasiri na upendo — watu wanaoonyesha kwa uwazi zaidi sura ya kweli ya Mungu.

**Basi na tuombe kwamba, kama Pentekoste ya kwanza ilivyokuwa, nasi tubadilishwe na Roho Mtakatifu, na kuwezeshwa kuwa mabalozi wa Kristo, tukishiriki upendo wa Mungu na wale watu wetu Watano.**



thykingdomcome.global